**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

---

# KIKAO CHA NUSU MWAKA CHA WIZARA NA WAKUU WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## AGENDA NA.2

## KUPOKEA TAARIFA KUHUSU FURSA ZOTE ZA UFADHILI WA MASOMO ZINAZOTARAJIWA KUTOLEWA KWA WATANZANIA ZIKIWEMO UFADHILI KUTOKA KWA WADAU MBALIMBALI IKIWEMO VYUO VIKUU, PAMOJA NA PROGRAMU YA SAMIA SCHOLARSHIP

# YALIYOMO


UFADHILI UNAOTOLEWA NA WIZARA PAMOJA NA WADAU KATIKA KUSOMESHA WATANZANIA KATIKA VYUO VYA NDANI NA NJE YA NCHI ... 3

1. UTANGULIZI ... 3

2. UFADHILI WA SAMIA ... 3

2.1 Ufadhili wa Samia Skolashipu kwa Vyuo vya Ndani ... 4

2.2 Ufadhili wa Samia Skolashipu Extended (DS/AI+) kwa Vyuo Bora Duniani ... 5

2.3 Ufadhili Wa Skolashipu Extended (Atomu) ... 7

3. FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NJE YA NCHI ... 7

4. UFADHILI KWA VYUO VIKUU VYA KIJERUMANI NCHINI MISRI ... 8

5. UFADHILI WA MAFUNZO KWA VITENDO ISRAEL - KILIMO ... 9

6. UFADHILI WA MASOMO KUPITIA MRADI WA HEET ... 10

6.1 Ufadhili wa Masomo kwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ... 10

6.2 Ufadhili wa Masomo ya Kozi Msingi Maalumu kwa Wasichana katika Fani za Sayansi ... 10

7. TAARIFA ZA FURSA ZA MASOMO NA UFADHILI KWA UMMA ... 11

8. USHAURI NA MAJIBU KWA WAOMBAJI ... 13

9.1 Mafanikio ... 14

9.3 Changamoto za kutokujaza nafasi tunazopewa ... 15

9.2 Changamoto Mahsusi kwa Skolashipu za Afrika ... 17

9.4 Utatuzi Unaopendekezwa ... 18

## UFADHILI UNAOTOLEWA NA WIZARA PAMOJA NA WADAU KATIKA KUSOMESHA WATANZANIA KATIKA VYUO VYA NDANI NA NJE YA NCHI

## 1. UTANGULIZI

Ufadhili wa elimu ni nyenzo muhimu katika kukuza rasilimali watu na kuharakisha maendeleo ya Taifa, hususan kwa kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira la ndani na la kimataifa. Kupitia jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuanzisha na kuimarisha fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo ya ndani na nje ya nchi, ikiwemo **Samia Scholarship**, **Samia Scholarship Extended**, fursa za masomo kutoka nchi rafiki, pamoja na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama **HEET**, kwa lengo la kuongeza upatikanaji, ubora na ushindani wa elimu ya juu, hususan katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) na Ubunifu.

Aidha, utekelezaji wa uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo unaongozwa na Mwongozo wa Kitaifa wa Kuongeza Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi, unaolenga kuongeza upatikanaji wa fursa hizo, kuweka utaratibu wa uratibu/usimamizi, na kuboresha utambuzi na ufuatiliaji wa wanufaika kwa maslahi ya taifa. Vilevile, Mkakati wa Kitaifa wa Umataifishaji wa Elimu unaelekeza kuboresha udahili na uandikishaji wa Watanzania kusoma nje ya nchi, kuimarisha utangazaji wa fursa, na kuweka mifumo bora ya ufuatiliaji wa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi.

## 2. UFADHILI WA SAMIA

Serikali imeanzisha Ufadhili wa Samia Scholarship katika maeneo makuu matatu, ambayo ni:

- Ufadhili wa masomo katika Vyuo Vikuu vya Ndani ya Nchi;
- Ufadhili wa masomo katika Vyuo Vikuu bora na vya Nje ya Nchi kwa masomo ya Data Science ,Artificial Intelliegence na Allied Science ; na

- Ufadhili wa masomo nje ya nchi kupitia **Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC)**.

## 2.1 Ufadhili wa Samia Skolashipu kwa Vyuo vya Ndani

Kuanzia mwaka wa fedha **2022/23**, Serikali imeanzisha **Ruzuku ya Samia Scholarship** kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita wanaosoma shahada katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Idadi ya wanufaika imeongezeka mwaka hadi mwaka:

**Jedwali Na. 1. Takwimu za Samia Scholashipu kwa Vyuo vya ndani**

| Mwaka wa Masomo | Jumla ya Wanafunzi | Wavulana | Wasichana |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 636 | 374 | 263 |
| 2023/24 | 1,228 | 756 | 472 |
| 2024/25 | 1,323 | 822 | 501 |

Kwa ngazi ya Uzamili, mwaka 2024/25 wanafunzi 80 (wavulana 50, wasichana 30) walipata ufadhili maalum wenye thamani ya **TZS milioni 623.2**. Taarifa hizi zinaonyesha dhamira ya Serikali ya kuwekeza katika ubora wa elimu ya juu, hasa katika fani za sayansi. Serikali imetenga shilingi 6,745,000,000 kwa ajili ya Ruzuku ya Samia Scholarship kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita wanaodahiliwa katika shahada za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM)**.**

Kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa ufadhili huu (**2022/2023)**, **wanafunzi 636 wa shahada** walipangiwa Kiasi cha **TZS 2,995,009,174**, ikijumuisha **wavulana 374 na wasichana 263**. Mwaka wa pili wa utekelezaji (**2023/2024)**, idadi ya wanafunzi waliopangiwa shahada iliongezeka hadi **1,228**, wakiwemo **918 wa mwaka wa kwanza na 310 wanaoendelea**, na kiasi cha mikopo **TZS 6,430,099,432** (wakiume 756, wakike 472).

Mwaka wa tatu wa utekelezaji (**2024/2025)**, wanafunzi waliopangiwa shahada walikuwa **1,323** ambapo wanafunzi wapya ni 647, na wanaoendelea 676 wakiwa na tengeo la **TZS 6,767,049,114**. Kwa upande wa **shahada ya uzamili**, mwaka **2024/2025** wanafunzi 80 (Wakiume 50, Wakike30) waliopangiwa na kupokea kiasi cha TZS. **TZS 623,200,000.**

Taarifa hii inaonesha **ongezeko la idadi ya wanafunzi na kiasi cha ruzuku** kwa miaka mitatu mfululizo, ikionesha uwekezaji mkubwa zaidi wa Serikali katika kuimarisha elimu ya juu hususani katika fani za STEM.

**Jedwali Na. 2. Takwimu za Wanafunzi wanufaika wa Ufadhili wa Masomo wa Samia**

| Mwaka wa Fedha | Program | Wanafunzi Waliopangiwa | Wanafunzi wa Kwanza | Wanafunzi Wanaoendelea | ME | KE | Jumla Wanafunzi | Kiasi cha Mikopo (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2022/2023 | Shahada | 636 | 636 | - | 374 | 263 | 636 | 2,995,009,174 |
| 2023/2024 | Shahada | 1,228 | 918 | 310 | 756 | 472 | 1,228 | 6,430,099,432 |
| 2024/2025 | Shahada | 1,323 | 647 | 676 | 822 | 501 | 1,323 | 6,767,049,114 |
| 2024/2025 | Uzamili | 80 | 80 | - | 50 | 30 | 80 | 623,200,000 |

## 2.2 Ufadhili wa Samia Skolashipu Extended (DS/AI+) kwa Vyuo Bora Duniani

Katika kuendelea kutekeleza azma yake ya kutoa elimu inayozingatia ujuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira na kuchangia katika maendeleo ya Taifa, Serikali imeanzisha programu maalum ya ufadhili wa Samia mahususi kwenye eneo la Sayansi ya Data, Akili Unde na Sayansi za mwelekeo huo ( Samia Scholarship Extended for Data Science, Artificial Intelligence (AI) and Allied Sciences (SSE DS/AI+) ili kutengeneza wataalamu mahiri katika fani hizo ambao watakuwa na uwezo mkubwa wa kushindana kitaaluma katika soko la ajira kitaifa, kikanda na kimataifa na kupata ajira au kujiajiri popote duniani**.** Programu hii inaratibiwa na **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)** na inatoa ufadhili unaojumuisha:

- Ada ya masomo;
- Posho ya kujikimu;
- Bima ya afya;
- Tiketi za ndege;
- Gharama za visa za masomo;

- Gharama za mitihani ya maandalizi (ikiwemo IELTS, SAT au mitihani mingine inayotakiwa);
- Gharama za udahili na usajili wa vyuo.

Wizara imeanza kwa kuwachukua wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu katika taasusi za PCM,PGM na PMC kutoka NECTA kwa ajili ya kwenda kusoma shahada ya kwanza katika vyuo bora vya nje ya nchi katika programu husika. Wanafunzi hao wako kambi ya mafunzo (Bootcamp) NM-AIST kwa ajili ya maandalizi ya kujiunga na vyuo Bora Duniani. Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeanza na wanufaika 50, ambapo:

- Wanafunzi **16** wanatarajiwa kuanza masomo katika Chuo Kikuu cha Johannesburg, Afrika Kusini tarehe 9 Februari 2026, na wanatarajiwa kuondoka nchini mnamo tarehe 1 Februari 2026 na wantarajiwa kusindikizwa na Mh. NWEST.
- Wanafunzi **34** wanatarajiwa kujiunga na vyuo mbalimbali nchini Ireland (Chuo Kikuu cha Limerick (UL) ; Chuo Kikuu Kishiriki cha Cork (UCC) na Chuo Kikuu kishiriki cha Dublin (UCD), na Technology University ya Dublin (TUD)

Wanafunzi hawa 34 waneendelea na mchakato wa kuomba Skolashipu katika vyuo vikuu bora duniani (Ona Kiambata na. 1 )

Aidha, programu hii inajumuisha ufadhili wa shahada ya uzamili kwa wanafunzi 20, wanaotarajiwa kusoma IITM Madrasa Zanzibar na NMAIST -Arusha kwa mgawanyo wa

- Wanafunzi 10 katika **Indian Institute of Technology (IIT) Madras – Zanzibar**; na
- Wanafunzi 10 katika **NM-AIST**,

kwa ajili ya kuendeleza taaluma katika maeneo ya Sayansi ya Data na Akili Unde iwapo watakidhi vigezo vya juu vya kupata ufadhili wa Samia. Aidha kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii, Serikali imetenga jumla ya TZS 5,487,252,869.

Vile vile , Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendeea kufanya mazungumzo na Mamlaka ya Saudi Arabia (Kingdom of Saudia Arabia) na Umoja wa Falme za Kiarabu (United Arab Emirates ) kuhusu ufadhili wa masomo na uwepo wa fedha za ufadhili ambazo Umoja wa Falme za Kiarabu umetenga kwa ajili ya nchi za Afrika hususani katika masuala ya Sayansi ya Data (Data Science), Akili Unde (Artificial Intelligence) na Sayansi Shirikishi (Allied Sciences).

### 2.3 Ufadhili Wa Skolashipu Extended (Atomu)

Kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi ya Nishati ya Atomu (Atomic energy) na pia nishati ya nyuklia (nuclear energy) katika maendeleo duniani kote WyEST ilianzisha fursa za kusomesha watanzania ubobezi wa fani hii katika nafasi ya umahiri katika Vyuo Vikuu bora Duniani. Programu hii ilianza mwaka 2024/25 ambapo serikali ilitenga jumla ya Tsh 1.5 bilioni kwa ajili ya ufadhili wa shahada za umahiri katika vyuo bora duniani katika maeneo ya *Nuclear Medicine, Medical Physics, Nuclear Engineering, Isotope hydrology* na mengine kama hayo.

Jumla ya skolashipu 6 zimeshatolewa ambapo kuanzia Oktoba 2025 Vijana wa Kitanzania walianza masomo katika Vyuo Vikuu vilivyopo Ufaransa, Uingereza, Afrika Kusini na Italy

## 3. FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NJE YA NCHI

Mojawapo ya majukumu ya Idara ya Elimu ya Juu ni kutafuta na kuratibu fursa mbalimbali za masomo na ufadhili nje ya nchi. Idara imekuwa ikishirikiana na kuratibu ufadhili wa masomo kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Hungaria, China, Uingereza, Urusi, Misri, Algeria, Mauritius, Morocco, Msumbiji Kupitia ushirikiano huo, jumla ya Watanzania wapatao 793 wamefaidika na ufadhili wa masomo kwa kipindi cha mwaka wa masomo 2020/2021 hadi 2025/2026, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3.

Aidha, Wizara ilipokea ufadhili wa nafasi 127 za masomo kutoka Saudi Arabia, ambao zilianza kutolewa kwa Watanzania katika mwaka wa masomo 2025/2026. Vilevile, Serikali ya Belarus imewasilisha ufadhili wa nafasi 3 za masomo zitakazotolewa katika mwaka wa masomo 2026/2027.

Hatua hizi ni sehemu ya utekelezaji wa umataifishaji wa elimu, unaolenga kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata fursa za kusoma nje ya nchi pamoja na kuongeza ufadhili unaowawezesha Watanzania kusoma nje ya nchi.

**Jedwali Na. 3. Takwimu za Wanufaika wa fursa za Ufadhili wa Masomo kutoka Nje ya Nchi Mwaka 2020/21 – 2025/26.**

| Na | Nchi | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | JML |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hungaria | 26 | 21 | 23 | 23 | 20 | 21 | 134 |
| 2 | China | 76 | 72 | 52 | 23 | 31 | 49 | 303 |
| 3 | Urusi | 20 | 25 | 50 | 90 | 90 | 150 | 425 |
| 4 | Commonwealth (UK) | 07 | 12 | 03 | 09 | 5 | 0 | 36 |
| 5 | Misri | 47 | 09 | 2 | 2 | 2 | 10 | 72 |
| 6 | Mauritius | 04 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 08 |
| 7 | Algeria | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 33 | 56 |
| 8 | Morocco | 34 | 26 | 0 | 0 | 0 | 04 | 64 |
| 9 | Msumbiji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 00 |
| 10 | Chevening (UK) | 0 | 0 | 0 | 17 | 5 | 0 | 22 |
| 11 | Ireland | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 10 |
| | | **214** | **165** | **130** | **166** | **178** | **277** | **1130** |
| | | **JUMLA KUU** | | | | | | **1130** |

## 4. UFADHILI KWA VYUO VIKUU VYA KIJERUMANI NCHINI MISRI

Kwa mwaka wa masomo 2025/2026 (Muhula wa Kipupwe – Spring Semester 2026), jumla ya wanafunzi wa Kitanzania kumi (10) wamefanikiwa kupata ufadhili wa masomo katika vyuo vikuu bora vya Kijerumani vilivyopo nchini Misri, baada ya kukidhi vigezo vya kitaaluma na ushindani vilivyowekwa na vyuo husika. Vyuo vya German International University (GIU) na German University in Cairo (GUC) ni miongoni mwa vyuo vikuu vinavyotambulika kimataifa, vinavyoendesha programu kwa viwango vya elimu ya juu vya Kijerumani, vikijikita katika mitaala ya kisasa, ubora wa ufundishaji, na uhusiano imara na vyuo vikuu na sekta za viwanda barani Ulaya.

Ufadhili huu unagharamia:

- Ada kamili za masomo;
- Tiketi moja ya ndege (kwenda na kurudi);
- Posho ya gharama za maisha; na
- Posho ya usafiri wa ndani.

Ufadhili huu utaanza rasmi katika Muhula wa Masika (Spring Semester 2026), unaotarajiwa kuanza tarehe 17 Februari 2026.

## 5. UFADHILI WA MAFUNZO KWA VITENDO ISRAEL - KILIMO

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kuratibu zoezi la kupeleka wanafunzi (wahitimu wa Vyuo vya Mafunzo ya kilimo na vyuo vikuu) kwenye program ya mafunzo ya kilimo kwa vitendo nchini Israel.

Mafunzo ya kilimo hutolewa kwenye mashamba makubwa nchini Israel yenye teknolojia za kisasa ili kuongeza ujuzi na weledi kwa vijana. Awali, toka mwaka 2015, mafunzo yaliratibiwa na Umoja wa Wahitimu Wajasiriamali Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUGECO) hadi mwaka 2019 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dr. John Joseph Pombe Magufuli alipoelekeza mafunzo yasimamiwe na Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano na wizara za kisekta chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Idadi ya wanafunzi wanaoshiriki mafunzo hayo imekuwa ikiongezeka kutoka wanafunzi 36 mwaka 2020 hadi wanafunzi 155 mwaka 2024 kama inavyoonekana kwenye jedwali 4. Aidha, kwa mwaka 2020 hadi 2024 Wanafunzi 781 wamenufaika na programu hii. Kwa mwaka 2025 WyEST inasubiri kupokea maelekezo ya mafunzo kutoka kwa mratibu wa Mafunzo ambaye ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika mashariki.

**Jedwali Na. 4. Takwimu za Wanafunzi wa Kitanzania walionufaika na programu ya mafunzo ya Kilimo kwa Vitendo nchini Israel toka mwaka 2020-2026**

| **Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **2026** | **JML** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi | 36 | 80 | 250 | 260 | 155 | **-** | **50** | **831** |

# 6. UFADHILI WA MASOMO KUPITIA MRADI WA HEET

## 6.1 Ufadhili wa Masomo kwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu

Wizara kupitia Mradi inasomesha wahadhiri 587 (wanawake 186 (31.7%) na wanaume 401 (68.3%) wa vyuo vya umma. Wahadhiri hawa wamewezeshwa kuendelea na masomo ya uzamili kupitia Mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi kwa Elimu ya Juu (HEET) ndani na nje ya nchi . Kati yao, 348 (59.3%) wamejiunga na programu za Shahada ya Uzamivu (PhD), huku 239 (40.7%) wakisoma Shahada ya Uzamili (Master's). Kati ya hao 161 (27.4%) wamehitimu masomo yao na 418 (70.8%) wako katika hatua mbalimbali za masomo yao, na walioshindwa masomo yao ni 10 (1.7%). Mradi wa HEET pia iumesomesha Wahadhiri 27 wa kada za Afya kutoka vyuo vikuu vya binafsi katika ngazi ya Umahiri (8) na Uzamivu (19).

## 6.2 Ufadhili wa Masomo ya Kozi Msingi Maalumu kwa Wasichana katika Fani za Sayansi

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mradi wa HEET inatoa ufadhili wa masomo katika ngazi ya **Foundation Programme** – (Special Foundation Course Scholarship for Female Science Students) kwa wasichana wanaotoka katika kaya maskini na yatima ambao wamepungukiwa kwa kiwango kidogo sifa za kujiunga na elimu ya juu katika fani za Sayansi. Ufadhili huu ni wa **asilimia 100**, unasimamiwa na Wizara na kutekelezwa na **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)**.

Lengo la ufadhili huu ni kuimarisha mpango mahususi wa Wizara wa **kuongeza idadi ya wasichana katika fani za Sayansi katika ngazi ya elimu ya juu**, ili kupunguza ombwe la wanasayansi wa kike katika fani za **Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STUH)**.

Sifa za kujiunga na ufadhili huu ni pamoja na mwombaji kuwa **Mtanzania wa kike**, mwenye **umri usiozidi miaka 35**, anayetoka katika kaya maskini zinazotambuliwa na **TASAF au Serikali ya Kijiji**, au awe ni **yatima**. Aidha, mwombaji awe amehitimu

**Kidato cha Sita** katika tahasusi za Sayansi hususan **PCB, PCM, CBG, PGM, CBA, PMC au CBN**, na kupata **pointi zisizopungua 1.5** kutoka kwenye masomo mawili. Kwa waombaji wa ngazi ya **Diploma**, wanatakiwa kuwa wamesoma fani za STUH na kupata **GPA isiyopungua 2.0 au wastani usiopungua daraja C**.

Utekelezaji wa programu hii ulianza rasmi mwaka wa masomo **2023/2024**, ambapo **wanafunzi 204** walidahiliwa. Kati yao, **wanafunzi 188** walifaulu mtihani wa mwisho, na **wanafunzi 176 (93.6%)** walipata udahili katika taasisi mbalimbali za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati (Diploma) nchini. Katika **awamu ya pili (2024/2025)**, programu ilisajili jumla ya **wanafunzi 260**, ambapo **wanafunzi 187 (71.9%)** walipata nafasi ya kujiunga na elimu ya juu nchini. **Awamu ya tatu ya utekelezaji** wa programu ilianza mwezi **Novemba, 2025**, ambapo wanafunzi wanaendelea na masomo yao.

Kwa kipindi cha miaka mitano, **tengeo la fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ufadhili huu ni Dola za Kimarekani Milioni Moja (USD 1,000,000)**.

Wanufaika wa ufadhili huu hupatikana baada ya **timu maalumu ya wataalamu**, kama ilivyoainishwa katika **Mwongozo wa Uendeshaji wa Programu**, kupitia na kuchambua maombi ya wanafunzi na kubaini waombaji wenye sifa stahiki. Mtaala unaotumika kufundishia programu hii ni **Mtaala wa Foundation Programme wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**, uliopitishwa na **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)**.

## 7. TAARIFA ZA FURSA ZA MASOMO NA UFADHILI KWA UMMA

Ili kuwezesha wananchi, hususan wanafunzi na wahitimu wa vyuo, kujiandaa mapema na kushiriki kikamilifu katika fursa za ufadhili wa masomo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweka utaratibu wa kutangaza ratiba za muda wa kufunguliwa na kufungwa kwa scholarship kulingana na kalenda za nchi na taasisi zinazotoa ufadhili. Ratiba hizi hutangazwa mapema kupitia tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii ya Serikali, pamoja na taasisi washirika, kwa lengo la:

- Kuwasaidia waombaji kupanga maandalizi ya nyaraka muhimu;
- Kupunguza ucheleweshaji na maombi yasiyokidhi vigezo;
- Kuongeza uwiano wa ushindani wa haki na uwazi;

- Kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanapata fursa ya kushiriki.

Aidha, waombaji wanatakiwa kutuma maombi yao kwenye email maalumu ambayo ni scholarship@moe.go.tz

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa, Wizara inaendelea kuboresha njia za kutangaza fursa ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii kwa uwazi na urahisi.

Jedwali lifuatalo linaonesha kwa muhtasari muda wa kawaida ambao skolashipu mbalimbali hufunguliwa na kufungwa, pamoja na mwaka wa masomo unaoanza:

**Jedwali Na. 5. Muda wa kufungua na kufunga ambao skolashipu kwa baadhi ya nchi**

| SN | Nchi | Jina la Ufadhili | Ngazi ya Masomo | Aina ya Ufadhili | Muda wa Maombi | Mwaka wa Masomo Unaonza |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | China | China Scholarship Council | Bachelor, Master, PhD | Full | Dec–Feb | Sept |
| 2 | Uingereza | Commonwealth Scholarship | Master, PhD | Full | Sept – Dec | Dec |
| 3 | Hungary | Stipendium Hungaricum | BA, MA, PhD | Full | Nov – Jan | Sept |
| 4 | Russia | Russia Scholarship | Bachelor, Master, PhD | Partial | Aug – Oct | Sept |
| 5 | Algeria | Algerian Government Scholarship | Bachelor | Partial | Jul – Sept | Sept |
| 6 | Morocco | Morocco Government Scholarship | Bachelor, Master, PhD | Partial | May – Jul | Sept |
| 7 | Egypt | Egyptian Government Scholarship | Bachelor | Partial | May – Jul | Sept |
| 8 | Mauritius | Mauritius–Africa Scholarship | Bachelor, Master, PhD | Full | Mar – Apr | Sept |
| 9 | Saudi Arabia | Study in Arabia Scholarship | Bachelor | Full | May – Jul | Sept |
| 10 | Oman | Sultanate of Oman Scholarship | Bachelor | Full | May – Jul | Sept |

## 8. USHAURI NA MAJIBU KWA WAOMBAJI

Idara hupokea na kushughulikia maswali ya waombaji kupitia: **barua pepe rasmi; simu; na maafisa wa Dawati la Elimu ya Juu.** Huduma hizi zinasaidia wananchi kuelewa vizuri masharti ya ufadhili, kuepuka taarifa potofu, na kufanya maamuzi sahihi kuhusu maombi ya masomo.

# 9. MAFANIKIO , CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

## 9.1 Mafanikio

Katika kipindi cha utekelezaji wa mipango ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepata mafanikio makubwa katika kutafuta, kuratibu na kusimamia fursa za ufadhili wa masomo nje ya nchi kwa Watanzania, hususan katika nchi za Afrika, Asia, Ulaya na Mashariki ya Kati.

Mafanikio haya yamechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha rasilimali watu, kuongeza upatikanaji wa elimu ya juu, na kujenga wataalamu wenye ujuzi unaohitajika katika maendeleo ya Taifa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kuongezeka kwa idadi ya Watanzania wanaonufaika na ufadhili wa masomo nje ya nchi, hususan katika nchi za Afrika kama Algeria, Morocco, Misri na Mauritius, jambo linalopanua wigo wa fursa za elimu kwa vijana wa Kitanzania;

(ii) Kuimarika kwa ushirikiano wa kielimu kati ya Tanzania na nchi rafiki kupitia makubaliano ya kiserikali na taasisi mbalimbali za elimu ya juu, hali iliyowezesha upatikanaji wa nafasi za masomo katika vyuo vinavyotambulika kimataifa;

(iii) Kuimarishwa kwa uratibu wa utoaji wa taarifa za scholarship kwa umma, ikiwemo kutangaza ratiba za muda wa ufadhili, vigezo vya sifa na taratibu za maombi kupitia mifumo rasmi ya Serikali;

(iv) Kuongezeka kwa uwezo wa Wizara kufuatilia na kusimamia masuala ya udahili, visa na vibali vya masomo kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Balozi za Tanzania katika nchi husika;

(v) Kuimarika kwa uwazi na usawa katika upatikanaji wa fursa za ufadhili kwa kutoa taarifa kwa wakati na kuwezesha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kushiriki kwa ushindani wa haki;

(vi) Kuongezeka kwa uelewa wa umma kuhusu fursa za masomo nje ya nchi, hali inayochochea ushindani, ubora wa waombaji na maandalizi ya mapema kwa wanafunzi.Kuandaa mfumo wa TEMIS ambao unatarajiwa

(vii) kuanzisha kanzidata ya kitaifa ya waombaji na wanufaika wa ufadhili wa masomo nje ya nchi kwa ajili ya ufuatiliaji, uwazi na upangaji bora wa sera, uchambuzi makini . Mfano kuna baadhi ya skolahipu huwa na waombaji wengi (Commonwealth UK – 445)

Kwa ujumla, mafanikio haya yanaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kupanua fursa za elimu ya juu nje ya nchi, kuimarisha diplomasia ya elimu, na kuhakikisha Watanzania wananufaika kikamilifu na ushirikiano wa kimataifa katika kujenga rasilimali watu bora.

## 9.3 Changamoto za kutokujaza nafasi tunazopewa

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiratibu fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo zinazotolewa na nchi/mashirika rafiki ya nje ya nchi. Kati ya fursa hizo, zipo zinazoratibiwa moja kwa moja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na nyingine huratibiwa na mawakala mbalimbali, ubalozi, sekta, taasisi nk. Aidha, baadhi ya fursa zinahitaji uratibu wa awali wa Wizara na hatua za mwisho za upendekezaji wa wanufaika hufanywa na nchi iliyotoa fursa za ufadhili. Hata hivyo, pamoja juhudi za Wizara ya kuratibu fursa hizo, zipo changamoto kadhaa zinazosababisha baadhi ya waombaji kukosa sifa.

**Changamoto zinazobainika Wakati wa Uchambuzi wa Maombi.**

Timu za Wizara zinazohusika na uchambuzi wa fursa mbalimbali za masomo zimekuwa zikibaini mapungufu kadhaa yanayowakwamisha waombaji kupata nafasi za ufadhili. Mambo hayo ni pamoja na:

i. Kutokujua au kutosoma matangazo kwa umakini – Waombaji wengi hushindwa kuelewa masharti na vigezo vilivyowekwa;

ii. Kutojiandaa mapema – Waombaji huanza mchakato wa maombi kwa haraka bila maandalizi ya awali;

iii. Kukosa viambatanisho muhimu – Maombi hutumwa bila nyaraka zinazohitajika (vyeti, barua za mapendekezo, nakala za hati za kusfairia n.k.);

iv. Fomu za maombi kutokamilika – Waombaji huacha sehemu muhimu za fomu bila kujazwa;

v. Matokeo yasiyo rasmi – Kutumia Provisional Results badala ya Transcripts zilizothibitishwa na vyuo husika;

vi. Waombaji wa PhD kukosa wasimamizi (supervisors) – Hii hupunguza uwezekano wa kukubalika;

vii. Ukosefu wa wadhamini (referees) – Waombaji wengi hawana barua za mapendekezo kutoka kwa wakufunzi au waajiri wao;

viii. Vyeti visivyothibitishwa – Wanafunzi waliosoma nje ya nchi kutokuambatisha uthibitisho wa vyeti kutoka NECTA, TCU au NACTVET;

ix. Kushindwa mitihani ya usahili – Baadhi ya vyuo huweka mitihani ya kuwapima waombaji;

x. Ubora hafifu wa maandiko – maandiko dhana ya tafiti (Concept notes na research proposal) zinazotarajiwa kufanywa na waombaji hazionyeshi uelewa wa kina au mchango wa kitaaluma;

xi. Kutozingatia vipaumbele vya taifa – Waombaji hushindwa kuonyesha namna masomo yao yatakavyosaidia kufikia malengo ya kitaifa; na

xii. Kutofanya mitihani ya lugha ya Kiingereza (TOEFL/IELTS) – Ambayo ni sharti kwa vyuo vingi vya kimataifa.

## 9.2 Changamoto Mahsusi kwa Skolashipu za Afrika

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika uratibu na utekelezaji wa ufadhili wa masomo nje ya nchi, bado zipo changamoto kadhaa zinazowakabili wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma katika baadhi ya nchi za Afrika. wanafunzi ( hususan Algeria, Morocco, Misri Na Mauritius). Changamoto hizi huathiri ustawi wa wanafunzi na ufanisi wa masomo, na hutofautiana kulingana na nchi husika. Changamoto hizo ni pamoja na:

(i) Kutokujaza nafasi tunazopewa kwenye baadhi ya nchi kutokana na sababu mbalimbali.

(ii) Kuchelewa kwa taarifa za fursa za ufadhili kufika Wizarani, hali inayowafanya baadhi ya waombaji kuwa tayari wamejiunga na vyuo vya ndani kabla ya taarifa hizo kupatikana;

(iii) Ufadhili wa masomo kutokuwa kamili na kushindwa kukidhi gharama halisi za maisha kama chakula, makazi, usafiri na mahitaji ya msingi ya kila siku;

(iv) Lugha za kufundishia, hususan Kiarabu au Kifaransa, ambazo si lugha mama kwa wanafunzi wengi wa Kitanzania, hali inayopunguza uelewa na ufanisi wa masomo;

(v) Mabadiliko ya masharti ya ufadhili baada ya wanafunzi kuwasili, ikiwemo kupunguzwa kwa posho au kutozwa gharama mpya zisizotarajiwa;

(vi) Ucheleweshaji wa posho za kujikimu, hali inayowaweka wanafunzi katika mazingira magumu ya maisha;

(vii) Changamoto za makazi na huduma za msingi, ikiwemo upatikanaji wa chakula, maji salama ya kunywa, intaneti na huduma za afya;

(viii) Tofauti za kiutamaduni na kijamii, mfano mila za chakula, mfumo wa maisha ya hosteli na mahusiano ya kijamii;

(ix) Mazingira ya hali ya hewa kama baridi kali au joto kali katika baadhi ya nchi, yanayoongeza gharama za maisha na mahitaji ya ziada kwa wanafunzi;

(x) Baadhi ya vyeti vya elimu kutotambulika na mamlaka za kitaifa za udhibiti wa elimu pindi wahitimu wanaporejea nchini;

(xi) Ukosefu wa takwimu sahihi za waombaji na wanufaika wa ufadhili kutokana na baadhi ya waombaji kuomba nje ya mifumo rasmi ya Serikali.

Changamoto hizi zinaonesha hitaji la kuimarisha uratibu wa wadau (Wizara–Balozi–taasisi husika) na mifumo ya ufuatiliaji wa wanafunzi na wanufaika.

### 9.4 Utatuzi Unaopendekezwa

Kukabiliana na changamoto zilizobainishwa na kuhakikisha mafanikio yaliyopatikana yanaendelea kuleta tija kwa Taifa, inapendekezwa kuchukuliwa hatua zifuatazo:

(i) Kuanzisha mfumo maalumu wa kukusanya na kutunza takwimu za elimu ya juu zikiwemo zile za ufadhili wa masomo unaojulikana kama TEMIS (Tertiary Education management Information System):

(ii) Elimu kwa umma kupitia vipindi vya Redio na Televisheni na maelezo ya ziada kwa waombaji wa fursa zinazotangazwa na wizara.

iii) Kuimarisha ufundishaji wa lugha katika kipindi cha elimu msingi(basic education) ;

(iv) Kuandaa mafunzo elekezi ya lugha, utamaduni na mazingira ya nchi husika kabla ya wanafunzi kuondoka nchini, ili kuwawezesha kuzoea mazingira ya masomo na maisha kwa haraka;

(v) Kufanya makubaliano ya maandishi na nchi zinazotoa ufadhili ili kuhakikisha masharti ya ufadhili yanabaki kama yalivyotangazwa na kuepuka mabadiliko yasiyotarajiwa baada ya wanafunzi kuwasili;

(vi) Kuimarisha ufuatiliaji wa masuala ya posho, makazi na huduma za msingi kwa wanafunzi walioko nje ya nchi kupitia Balozi za Tanzania;

(vii) Kuimarisha ushauri na msaada wa kijamii kwa wanafunzi kupitia mifumo ya mawasiliano na ushirikiano kati ya Wizara, Balozi na wanafunzi; na

vii) Kuimarisha uratibu kati ya Wizara ya Elimu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Balozi za Tanzania ili taarifa za fursa za ufadhili zipatikane mapema na kwa wakati;

x) Kuimarisha ushiriki wa Balozi katika kubaini fursa, kuratibu taarifa za wanufaika, na kutoa usaidizi wa kijamii/kiutamaduni kwa wanafunzi katika nchi husika.

xi) Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa maendeleo ya kitaaluma na kijamii kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi kwa kushirikiana na Balozi.

**KIAMBATA 1 : SUMMARY OF UNIVERSITY APPLICATIONS SUBMITTED BY BENEFICIARIES OF SSE SCHOLARSHIP WHO ARE AT THE BOOTCAMP**

| S/N | Student's Name | SOUTH AFRICA | NORTH AMERICA | ASIA & AUSTRALLIA | EUROPE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Abdulkarim Ibrahim Dahal | University of Johannesburg | NYU Abu Dhabi | Hong Kong University of Science and Technology | Queens University Belfast, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>Middlesex University, UK |
| 2 | Abel Reuben Lohelo | | York University | | Newcastle University, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>University of Bristol, UK<br>University College London, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 3 | Allen Lukelo Mahobe | | University of Waterloo | | University of Bristol, UK<br>Cardiff University, UK<br>Newcastle University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 4 | Anita Sosthenes Kulwa | | York University | | University of Birmingham, UK<br>Cardiff University, UK<br>University of Glasgow, UK<br>University of Sunderland, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 5 | Anjela Hector Mongi | | University of Rochester<br>McGill University | | University of Exeter, UK<br>University of Surrey, UK<br>London School of Economics and Political Science, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland<br>University College Dublin, Ireland |
| 6 | Boneventure Gerald Maliti | University of Johannesburg | University of British Columbia | | University of Birmingham, UK<br>Cardiff University, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Abertay University, UK<br><br>Cardiff Metropolitan University, UK<br><br>University of Hertfordshire, UK |
| 7 | Christina Peter Kessy | | University of Waterloo | | Newcastle University, UK<br><br>Heriot-Watt University, UK<br><br>University of Leeds, UK<br><br>Coventry University, UK<br><br>Middlesex University, UK<br><br>Limerick University, Ireland<br><br>University College Cork, Ireland |
| 8 | Colman Musa Muya | | | | University of Bristol, UK<br><br>Heriot-Watt University, UK<br><br>Newcastle University, UK<br><br>University of Sunderland, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 9 | Curthbert Junior Mushi | | | | University of Warwick, UK<br>University of Leeds, UK<br>University of Glasgow, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>Leeds Beckett University, Uk<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland<br>University College Dublin, Ireland<br>Bocconi University, Italy |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | Daniel Nicolaus Nhondya | | | Chinese University of Hong Kong | University of Leicester, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Wolverhampton, UK<br>Leeds Beckett University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 11 | Daniel Sumka Mbuba | | | | University of Leicester, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>UWE Bristol, UK<br>University of Sunderland, UK<br>Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland<br>University of Amsterdam, Netherland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 12 | David Furahini Vahaye | | | University of Technology Sydney | University of Leicester, UK<br>Bangor University, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 13 | David Sauwa Ulomi | | | Nanyang Technical University | University of Leicester, UK<br>University of Bristol, UK<br>UWE Bristol, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Edmund Livin Masawe | | Howard University<br>Michigan State University | | University of Warwick, UK<br>University of Surrey, UK<br>Newcastle University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland<br>University College Dublin, Ireland |
| 15 | Elia Enock Deus | University of Johannesburg | | City University of Hong Kong | University of Leicester, UK<br>London School of Economics and Political Science, UK<br>UWE Bristol, UK<br>Imperial College London, UK<br>Middlesex University, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 16 | Elia Richard Macha | | University of Calgary | | University of Leicester, UK<br>Bangor University, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>University of Bristol, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 17 | Emmanuel Freddy Mhegele | | York University | | University of Bristol, UK<br>London School of Economics and Political Science, UK<br>Cardiff University, UK<br>Coventry University, UK<br>Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 18 | Emmanuel Said Paul | | | University of Sydney | Newcastle University, UK<br>Aston University Birmingham, UK<br>Abertay University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>Leeds Beckett University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 19 | Frank Vicent Mwita | | McGill University | | University of Leicester, UK<br>Bangor University, UK<br>University of Birmingham, UK<br>University of Sunderland, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 20 | George Daud Pagija | | Howard University<br>Michigan State University | | University of Leicester, UK<br>Bangor University, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 21 | Gloria Charles Tundui | University of Johannesburg | | University of Hong Kong | University of Birmingham, UK<br>University of Leeds, UK<br>London School of Business, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Hertfordshire, UK |
| 22 | Godfrey Geofrey Ngaladzi | University of Johannesburg | Massachusetts Institute of Technology,<br>Stanford University, | Peking University | University of Warwick, UK<br>Cardiff University, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | University of Pennsylvania, Tufts University | | Nottingham Trent University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Hertfordshire, UK |
| 23 | Halid Rashid Halid | University of Johannesburg | | National University of Singapore | University of Leicester, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>Middlesex University, UK |
| 24 | Hezron Pauline Butemi | University of Johannesburg | | Hong Kong University of Science and Technology | University of Bristol, UK<br>University of Surrey, UK<br>University of Exeter, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Hertfordshire, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 25 | John Elifuraha Mziray | | | | Queens University Belfast, UK<br>Bangor University, UK<br>UWE Bristol, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland<br>Delft University of Technology, Netherlands |
| 26 | John Zabron Kwilasa | | | Chinese University of Hong Kong | Queens University Belfast, UK<br>Aston University Birmingham, UK<br>UWE Bristol, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>Leeds Beckett University, UK<br>Limerick University, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Technological University Dublin, Ireland |
| 27 | Jonathan Mulingwa Fimbo | University of Johannesburg | Amherst College<br>Yale University<br>Cornell University | Tsinghua University | University of Bristol, UK<br>University of Leeds, UK<br>University College London, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Plymouth, UK |
| 28 | Joshua Lazaro Jiyuga | University of Johannesburg | McGill University | | University College London, UK<br>Cardiff University, UK<br>UWE Bristol, UK<br>University of Sunderland, UK<br>Middlesex University, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 29 | Kelvin Mtayuga Hosea | | Northwestern University<br>Carnegie Mellon University<br>Bates College | | University College London, UK<br>University of Exeter, UK<br>Abertay University, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland<br>University College Dublin, Ireland |
| 30 | Khamis Hussein Simba | | | City University of Hong Kong | Queens University Belfast, UK<br>Bangor University, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | University College Cork, Ireland |
| 31 | Luqman Mjengi Malanga | University of Johannesburg | | University of Sydney | Queens University Belfast, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>UWE Bristol, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Hertfordshire, UK |
| 32 | Malaika Florence Wankanga | University of Johannesburg | | Nanyang Technological University | University of Leeds, UK<br>London School of Economics and Political Science, UK<br>University of Exeter, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Hertfordshire, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 33 | Martha Nkwimba Bonevanture | University of Johannesburg | Tufts University<br>University of Waterloo<br>Bates College | | University of Exeter, UK<br>University of Glasgow, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>De Mont Fort University, UK<br>Middlesex University, UK |
| 34 | Martin Menas Mathew | | University of Alberta | | University of Warwick, UK<br>Bangor University, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>Leeds Beckett University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 35 | Mathayo Simon Manamba | | | National University Singapore | Queens University Belfast, UK<br>University of Warwick, UK<br>Birmingham City University, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 36 | Nassor Shaibu Nassoro | | | University of Hongkong | Queens University Belfast, UK<br>Bangor University, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 37 | Obrien Cassian Kigeso | | | National University of Singapore | University College London, UK<br>University of Surrey, UK<br>Newcastle University, UK<br>University of Sunderland, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 38 | Omary Habibu Abdallah | | | University of Melbourne | University of Leicester, UK<br>Queens University Belfast, UK<br>UWE Bristol, UK<br>Coventry University, UK<br>Middlesex University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 39 | Richard Aldo Makendi | | | | University College London, UK<br>London School of Business, UK<br>Birmingham City University, UK<br>University of Sunderland, UK<br>University of Buckingham, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technical University Dublin, Ireland<br>KTH Royal Institute, Sweden |
| 40 | Rodgers Lucas Richard | | University of British Columbia | | University of Bristol, UK<br>Cardiff University, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>University of Wolverhampton, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | University College Cork, Ireland |
| 41 | Sabrina Said Hamisi | University of Johannesburg | | Monash University | University of Warwick, UK<br>University of Leeds, UK<br>London School of Business, UK<br>University of Sunderland, UK<br>Middlesex University, UK |
| 42 | Samson Thomas Nhegeji | | | Chinese University of Hong Kong | University of Leicester, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>University of Wolverhampton, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Technological University of Dublin, Ireland |
| 43 | Sangalu Mahinuka James | | Arizona State University<br>Howard University | | University of Leicester, UK<br>Aston University Birmingham, UK<br>Robert Gordon University, UK<br>Coventry University, UK<br>University of Buckingham, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University of Dublin, Ireland |
| 44 | Saverin Aganyira Samson | University of Johannesburg | University of Waterloo | | Queens University Belfast, UK<br>Bangor University, UK<br>Nottingham Trent University, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | University of Sunderland, UK<br>University of Plymouth, UK |
| 45 | Shadrack Leonard Hala | | Penn State University | | Heriott-Watt University, UK<br>University of Surrey, UK<br>Abertay University, UK<br>Coventry University, UK<br>Leeds Beckett University, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |
| 46 | Simon Aswile Simon | University of Johannesburg | University of Alberta | | University of Warwick, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>Birmingham City University, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Plymouth, UK |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 47 | Stewart Ludan Maliti | | University of Illinois Chicago<br>Howard University | | University of Birmingham, UK<br>University of Glasgow, UK<br>University of Exeter, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Hertfordshire, UK<br>Limerick University, Ireland<br>University College Cork, Ireland |
| 48 | Tomson Elibariki Julius | | | | Queens University Belfast, UK<br>University of Leicester, UK<br>UWE Bristol, UK<br>University of Sunderland, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 49 | Vicent Eliamini Swai | University of Johannesburg | | City University of Hong Kong | Queens University Belfast, UK<br>University of Leicester, UK<br>Nottingham Trent University, UK<br>University of Sunderland, UK<br>Middlesex University, UK |
| 50 | Zabron Michael Mwami | | University of Alberta | | Queens University Belfast, UK<br>Heriot-Watt University, UK<br>UWE Bristol, UK<br>Cardiff Metropolitan University, UK<br>University of Plymouth, UK<br>Limerick University, Ireland<br>Technological University Dublin, Ireland |